

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA NISHATI



MAMLAKA YA UDHIBITI WA
HUDUMA ZA NISHATI NA MAJI
(EWURA)



KUMB: PPR/2024 - 09/01

**TAARIFA KWA UMMA KUHUSU BEI KIKOMO ZA BIDHAA ZA MAFUTA YA
PETROLI KUANZIA JUMATANO, TAREHE 4 SEPTEMBER 2024**

Mamlaka ya Udhhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), inatangaza bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli hapa nchini zitakazotumika kuanzia **Jumatano ya tarehe 4 Septemba 2024 saa 6:01 usiku**. Kwa mwezi Septemba 2024, bei za rejareja na za jumla katika Mikoa ya Dar es Salaam, Tanga na Mtwara ni kama zinavyoonekana katika **Jedwali Na. 1 na 2**, mtawalia.

Jedwali 1: Bei Kikomo za Rejareja (Shilingi/Lita)

Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Dar es Salaam	3,140	3,011	3,121
Tanga	3,141	3,020	3,167
Mtwara	3,142	3,021	3,194

Jedwali 2: Bei Kikomo za Jumla (Shilingi/Lita)

Bandari	Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
Dar es Salaam	3,008.20	2,879.26	2,989.87
Tanga	3,009.25	2,888.65	-
Mtwara	3,010.52	2,889.53	-

Bei za mafuta za rejareja kwa maeneo mbalimbali ya miji, wilaya na mikoa ni kama zinavyooneshwa katika **Jedwali Na. 3**.

MWENENDO WA BEI ZA MAFUTA KATIKA SOKO LA DUNIA

Bidhaa za mafuta zinazoagizwa na kupokelewa nchini zinazingatia bei za mafuta yaliyosafishwa (FOB) kutoka soko la Uarabuni. Mwezi Septemba 2024, bei kikomo za mafuta zimekokotolewa kwa kuzingatia bei za soko la Uarabuni za mwezi Agosti 2024. Kwa kulinganisha na bei za Julai 2024, bei za Agosti 2024 za petroli, dizeli na mafuta ya taa zimepungua kwa wastani wa 7.68%, 6.22% na 6.20%, mtawalia.

MWENENDO WA GHARAMA ZA UAGIZAJI

Gharama za uagizaji wa mafuta (*premiums*) zimepungua kwa wastani wa 10.55% kwa petroli na 13.64% kwa dizeli na kuongezeka kwa 3.37% kwa mafuta ya taa katika Bandari ya Dar es Salaam; zimepungua kwa wastani wa 4.46% kwa petroli na dizeli katika Bandari ya Tanga; na zimepungua kwa wastani wa 14.98% kwa mafuta ya petroli na dizeli katika Bandari ya Mtwara.

VIWANGO VYA KUBADILISHA FEDHA ZA KIGENI

Gharama za mafuta yanayopokelewa (FOB) na gharama za uagizaji (*premiums*) hulipiwa kwa kutumia fedha za kigeni ikiwemo Dola ya Marekani. Kwa bei za mwezi Septemba 2024, wastani wa gharama za kubadilisha fedha za kigeni (*Applicable Exchange Rate*) umepungua kwa 0.91%. Wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa rejareja wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zinazooneshwa katika **Jedwali Na. 3**. Aidha, wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla wanatakiwa kuuza mafuta kwa bei zinazooneshwa katika **Jedwali Na. 2. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa dhidi ya mfanyabiashara yoyote atakayekiuka AGIZO hili.**

EWURA inapenda kuwakumbusha wafanyabiashara wa bidhaa za mafuta kwa jumla na rejareja pamoja na jamii kuzingatia yafuatayo: -

- a) bei kikomo za bidhaa za mafuta ya petroli kwa eneo husika zinapatikana kupitia simu za mkononi kwa kupiga namba ***152*00#** na kisha kufuata maelekezo. Huduma hii ni bure na inapatikana kupitia mitandao yote ya simu za mkononi hapa nchini.
- b) Kwa mujibu wa **Sheria ya Mafuta ya mwaka 2015, kifungu namba 166**, bei za bidhaa za mafuta ya petroli zitaendelea kupangwa na soko. EWURA itaendelea kuhamasisha ushindani kwa kutoa taarifa za bei kikomo za bidhaa za mafuta.
- c) Kampuni za mafuta ziko huru kuuza bidhaa za mafuta ya petroli kwa bei ya ushindani isipokuwa **bei hizo zisizidi bei kikomo (*Price cap*) au kuwa chini ya bei iliyoruhusiwa (*Floor Price*)** kama zilivyokokotolewa kwa mujibu wa **Kanuni za EWURA za Kupanga Bei za Mafuta za Mwaka 2022 zilizotangazwa tarehe 28 Januari 2022** kupitia **Gazeti la Serikali Na. 57** na marekebisho ya **Kanuni tajwa kupitia Gazeti la Serikali Na. 761A** la tarehe 30 Oktoba 2023 na **Mabadiliko ya Kanuni za Uagizaji wa Mafuta kwa Pamoja za Mwaka 2024**.
- d) Vituo vyote vya mafuta vinatakiwa kuchapisha bei za bidhaa za mafuta katika mabango yanayoonekana bayana yakionesha bei za mafuta, punguzo, vivutio vya kibiashara vinavyotolewa na kituo husika. Pale ambapo inawezekana kuchagua, wateja wanashauriwa kununua bidhaa za mafuta katika vituo vinavyouza mafuta kwa bei nafuu zaidi ili kushamirisha ushindani. **Wateja wanaweza kutoa taarifa za kituo chochote kinachouza mafuta juu ya bei kikomo kwa kupiga simu ya bure namba 0800110030 au kwa kuwasilisha kwa maandishi kupitia Ofisi za EWURA au kwa kutuma baruapepe kupitia info@ewura.go.tz. Ni kosa kuuza mafuta bila kuweka mabango ya bei inayoonekana vizuri kwa wateja. Adhabu kali itatolewa kwa kituo husika kwa kutotekeleza matakwa ya kisheria kwa mujibu wa kanuni husika.**
- e) Wauzaji wa bidhaa za mafuta ya petroli wanatakiwa kutoa stakabadhi za mauzo kutoka kwenye *Electronic Fiscal Pump Printers (EFPP)* na wanunuzi wahakikishe wanapata stakabadhi hizo za malipo zinazoonyesha jina la kituo, tarehe, aina ya mafuta yaliyonunuliwa na bei kwa lita. Stakabadhi hizo zitatumiwa kama kidhibiti kwa wanunuzi wa mafuta endapo kutajitokeza malalamiko ya kuuziwa mafuta kwa bei ya juu kuliko bei kikomo au kuuziwa mafuta yasiyo na kiwango cha ubora unaotakiwa. Stakabadhi hizo pia zitasaidia kurahisisha ukusanyaji wa kodi za Serikali zitokanazo na mauzo ya bidhaa za mafuta ya petroli.

JEDWALI NA. 3: BEI KIKOMO ZA REJAREJA – SHILINGI/LITA

Na	Mji	Bei Kikomo		
		Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
1	Dar es Salaam	3,140	3,011	3,121
2	Arusha	3,198	3,077	3,206
3	Arumeru (Usa River)	3,198	3,077	3,206
4	Karatu	3,216	3,095	3,224
5	Longido	3,209	3,088	3,216
6	Monduli	3,203	3,082	3,211
7	Monduli-Makuyuni	3,208	3,087	3,216
8	Ngorongoro (Loliondo)	3,282	3,162	3,297
9	Pwani (Kibaha)	3,144	3,016	3,126
10	Bagamoyo	3,151	3,022	3,132
11	Bagamoyo (Miono)	3,182	3,053	3,163
12	Bagamoyo (Mbwewe)	3,163	3,034	3,144
13	Chalinze Junction	3,154	3,025	3,135
14	Chalinze Township (Msata)	3,158	3,029	3,140
15	Kibiti	3,160	3,031	3,142
16	Kisarawe	3,147	3,018	3,128
17	Mkuranga	3,150	3,021	3,131
18	Rufiji	3,168	3,039	3,149
19	Dodoma	3,199	3,070	3,180
20	Bahi	3,206	3,077	3,187
21	Chamwino	3,194	3,065	3,175
22	Chemba	3,225	3,096	3,207
23	Kondoa	3,232	3,103	3,213
24	Kongwa	3,196	3,067	3,177
25	Mpwapwa	3,200	3,071	3,181
26	Mpwapwa (Chipogoro)	3,212	3,083	3,193
27	Mtera (Makatopora)	3,218	3,089	3,199
28	Mvumi	3,205	3,076	3,187
29	Geita	3,305	3,176	3,287
30	Bukombe	3,294	3,165	3,276
31	Chato	3,326	3,198	3,308
32	Mbogwe	3,344	3,215	3,325
33	Nyang'hwale	3,320	3,192	3,302
34	Iringa	3,204	3,075	3,185
35	Ismani	3,209	3,080	3,191
36	Kilolo	3,209	3,080	3,190
37	Mufindi (Mafinga)	3,214	3,085	3,195
38	Mufindi (Igowole)	3,223	3,094	3,204
39	Mufindi (Mgololo)	3,226	3,097	3,208
40	Kagera (Bukoba)	3,356	3,227	3,337
41	Biharamulo	3,330	3,201	3,311
42	Karagwe (Kayanga)	3,372	3,243	3,353
43	Kyerwa (Ruberwa)	3,378	3,249	3,359
44	Muleba	3,356	3,227	3,337
45	Ngara	3,343	3,214	3,325
46	Misenyi	3,364	3,235	3,345
47	Katavi (Mpanda)	3,298	3,169	3,279
48	Mlele (Inyonga)	3,279	3,150	3,261
49	Mpimbwe (Majimoto)	3,317	3,188	3,298
50	Tanganyika (Ikola)	3,316	3,187	3,297
51	Kigoma	3,302	3,173	3,284

Na	Mji	Bei Kikomo		
		Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
52	Uvinza (Lugufu)	3,293	3,164	3,274
53	Muyobozi Village (Uvinza)	3,304	3,175	3,286
54	Ilagala Village (Uvinza)	3,307	3,178	3,288
55	Buhigwe	3,301	3,172	3,282
56	Kakonko	3,303	3,174	3,285
57	Kasulu	3,311	3,183	3,293
58	Kibondo	3,309	3,180	3,290
59	Kilimanjaro (Moshi)	3,187	3,067	3,195
60	Hai (Bomang'ombe)	3,191	3,070	3,198
61	Mwanga	3,180	3,060	3,188
62	Rombo (Mkuu)	3,204	3,083	3,216
63	Same	3,174	3,053	3,181
64	Siha (Sanya Juu)	3,194	3,073	3,202
65	Lindi	3,156	3,035	3,180
66	Lindi-Mtama	3,160	3,039	3,198
67	Kilwa Masoko	3,180	3,059	3,155
68	Liwale	3,191	3,070	3,201
69	Nachingwea	3,176	3,055	3,209
70	Ruangwa	3,182	3,061	3,211
71	Manyara (Babati)	3,232	3,111	3,244
72	Hanang (Katesh)	3,242	3,122	3,254
73	Kiteto (Kibaya)	3,247	3,126	3,255
74	Mbulu	3,244	3,124	3,257
75	Simanjiro (Orkasumet)	3,264	3,143	3,276
76	Mara (Musoma)	3,306	3,177	3,287
77	Musoma Vijijini (Busekela)	3,318	3,190	3,300
78	Rorya (Ingirijuu)	3,313	3,184	3,294
79	Rorya (Shirati)	3,321	3,192	3,302
80	Bunda	3,297	3,168	3,279
81	Bunda (Kisorya)	3,309	3,181	3,291
82	Butiama	3,303	3,174	3,284
83	Serengeti (Mugumu)	3,314	3,185	3,296
84	Tarime	3,314	3,185	3,296
85	Tarime (Kewanja/Nyamongo)	3,320	3,191	3,301
86	Mbeya	3,247	3,118	3,228
87	Chunya	3,257	3,128	3,238
88	Chunya (Makongolosi)	3,262	3,133	3,243
89	Chunya (Lupa Tingatinga)	3,264	3,135	3,245
90	Kyela	3,263	3,134	3,244
91	Mbarali (Rujewa)	3,231	3,102	3,213
92	Rujewa (Madibira)	3,245	3,116	3,226
93	Rujewa (Kapunga)	3,241	3,112	3,222
94	Rungwe (Tukuyu)	3,256	3,127	3,237
95	Busokelo (Iwangwa)	3,265	3,136	3,246
96	Morogoro	3,165	3,036	3,146
97	Mikumi	3,181	3,052	3,162
98	Kilombero (Ifakara)	3,203	3,074	3,184
99	Kilombero (Mlimba)	3,225	3,096	3,207
100	Kilombero (Mngeta)	3,214	3,085	3,196
101	Ulanga (Mahenge)	3,213	3,085	3,195
102	Malinyi	3,224	3,095	3,205
103	Kilosa	3,183	3,054	3,165

Na	Mji	Bei Kikomo		
		Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
104	Gairo	3,183	3,054	3,165
105	Mvomero (Wami Sokoine)	3,175	3,046	3,157
106	Mvomero (Sanga Sanga)	3,165	3,036	3,146
107	Turian	3,190	3,061	3,171
108	Mtwara	3,142	3,021	3,194
109	Nanyumbu (Mangaka)	3,178	3,058	3,243
110	Masasi	3,158	3,037	3,219
111	Newala	3,163	3,042	3,226
112	Tandahimba	3,156	3,035	3,219
113	Nanyamba	3,156	3,035	3,219
114	Mwanza	3,290	3,161	3,271
115	Kwimba	3,308	3,179	3,289
116	Magu	3,298	3,169	3,280
117	Misungwi	3,285	3,156	3,266
118	Misungwi (Mbarika)	3,295	3,166	3,276
119	Sengerema	3,323	3,194	3,304
120	Ukerewe	3,350	3,221	3,331
121	Njombe	3,232	3,104	3,214
122	Luponde	3,239	3,110	3,220
123	Njombe (Kidegembye)	3,253	3,124	3,234
124	Ludewa	3,270	3,141	3,252
125	Makambako	3,225	3,096	3,206
126	Makete	3,263	3,134	3,245
127	Wanging'ombe (Igwachanya)	3,230	3,101	3,212
128	Rukwa (Sumbawanga)	3,313	3,184	3,294
129	Sumbawanga Rural (Mtowisa)	3,313	3,184	3,294
130	Kalambo (Matai)	3,320	3,191	3,302
131	Nkasi (Namanye)	3,326	3,198	3,308
132	Kabwe	3,341	3,212	3,322
133	Nkasi (Kirando)	3,336	3,207	3,317
134	Ruvuma (Songea)	3,228	3,107	3,245
135	Mbinga	3,240	3,119	3,257
136	Namtumbo	3,219	3,098	3,250
137	Nyasa (Mbamba Bay)	3,266	3,145	3,268
138	Tunduru	3,193	3,072	3,225
139	Shinyanga	3,269	3,140	3,250
140	Kahama	3,273	3,144	3,255
141	Kishapu	3,277	3,148	3,258
142	Ushetu (Nyamilangano)	3,285	3,156	3,267
143	Ushetu (Kangeme Village)	3,291	3,162	3,272
144	Salawe	3,283	3,154	3,264
145	Simiyu (Bariadi)	3,287	3,158	3,268
146	Busega (Nyashimo)	3,299	3,170	3,280
147	Itilima (Lagangabilili)	3,287	3,158	3,268
148	Maswa	3,281	3,152	3,262
149	Meatu (Mwanhuzi)	3,292	3,163	3,273
150	Singida	3,231	3,102	3,212
151	Iramba	3,243	3,114	3,224
152	Manyoni	3,215	3,086	3,197
153	Itigi (Mitundu)	3,231	3,102	3,212
154	Ikungi	3,226	3,097	3,208
155	Mkalama (Nduguti)	3,255	3,126	3,237

Na	Mji	Bei Kikomo		
		Petroli	Dizeli	Mafuta ya Taa
156	Songwe (Vwawa)	3,256	3,127	3,238
157	Songwe (Mkwajuni)	3,263	3,134	3,245
158	Ileje	3,260	3,131	3,242
159	Momba (Chitete)	3,265	3,137	3,247
160	Tunduma	3,261	3,132	3,242
161	Tabora	3,248	3,119	3,230
162	Igunga	3,248	3,119	3,229
163	Kaliua	3,261	3,132	3,243
164	Ulyankulu	3,259	3,130	3,240
165	Nzega	3,259	3,130	3,240
166	Sikonge	3,257	3,128	3,238
167	Urambo	3,258	3,129	3,239
168	Uyui	3,255	3,126	3,236
169	Mpyagula	3,280	3,151	3,261
170	Tanga	3,141	3,020	3,167
171	Handeni	3,162	3,041	3,147
172	Kilindi	3,177	3,056	3,181
173	Korogwe	3,153	3,033	3,160
174	Lushoto	3,163	3,042	3,170
175	Lukozi	3,168	3,048	3,175
176	Bumbuli	3,172	3,051	3,179
177	Mkinga (Maramba)	3,148	3,027	3,182
178	Muheza	3,146	3,025	3,167
179	Pangani	3,148	3,028	3,174

Dkt. James A. Mwainyekule
MKURUGENZI MKUU – EWURA